

# HALMASHAURI YA MANISPAA MTWARA-MIKINDANI



## TANGAZO LA ZABUNI YA HUDUMA YA ULINZI WA SILAHA (BUNDUKI) KWENYE MAENEO YA MANISPAA YA MTWARA MIKINDANI

25/05/2017

ZABUNI NA.LGA/085/2017/2018/NC/02

Halmashauri ya Manispaa Mtwara-Mikindani inakaribisha maombi kwa makampuni mbalimbali yenye sifa ya kufanya kazi za ulinzi wa kutumia silaha za moto (bunduki) kwenye malindo ya Halmashauri ya Manispaa Mtwara Mikindani kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

### MASHARTI YA MAOMBI YA ZABUNI

1. Nyaraka za maombi ya zabuni zitapatikana baada ya kulipa ada ya zabuni ya shilingi laki moja (100,000/=) tu. Ada hiyo haitarejeshwa (Non refundable).
2. Ombi la zabuni liwe na jina na anuani ya mwombaji na ataje kiasi atakacholipwa na Manispaa kwa mwezi ikiwa ni gharama za ulinzi wa silaha (bunduki) kwenye maeneo husika ndani ya Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara Mikindani..
3. Mwombaji anatakiwa awe na leseni hai ya huduma ya ulinzi iliyosajiliwa na mamlaka husika, awe na uthibitisho wa uzoefu wa kazi husika na uthibitisho wa uwepo wa stakabadhi za kielektroniki.
4. Maombi(halisi na nakala mbili) yafungwe kwenye bahasha ya khaki (A4) yenye lakiri na itumwe kwenye Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa kwa anuani ifuatayo:-

**Katibu wa Bodi ya Zabuni,  
Halmashauri ya Manispaa Mtwara-Mikindani  
S. L. P. 92  
MTWARA**

5. Kabrasha la maombi ya zabuni linapatikana katika ofisi ya Halmashauri ya Manispaa Mtwara-Mikindani kwa Katibu wa Bodi ya Zabuni, kuanzia saa 1.30 asubuhi mpaka saa 9.30 kwa siku za kazi (Jumatatu - Ijumaa).  
Mwisho wa kupokea maombi hayo ni tarehe 16/06/2017saa nne (4.00) asubuhi.  
Waombaji au wawakilishi wao wanaalikwa kuhudhuria ufunguzi wa zabuni katika ukumbi wa mikutano wa Manispaa.

**(SAMBWE P. SIJABAJE)  
KAIMU MKURUGENZI WA MANISPAA  
MTWARA-MIKINDANI**

